# SUZA kuanzisha Kigoda cha Karume kuenzi mchango wake

Maliki Muunguja, Mwananchi

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) katika kutekeleza majukumu yake kama Taasisi ya Elimu ya Juu nchi, kimedhamiria kuzindua Kigoda cha Kiitaaluma cha Hayat Sheikh Abeid Amani Karume.

Lengo kuu likiwa ni kuhifadhi, kuenzi na kendeleza mawazo na fikra za Sheikh Abeid Amani Karume katika kuleta ukombozi na maendeleo ya Zanzibar, Tanzania, Afrika na dunia kwa ujumla.

Hayo yote yatawezekana kupitia utafiti na mijadala mbalimbali ya kisomi itayosimamiwa na wadau na wataalam wa utafiti wa kada mbalimbali yenye muelekeo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kisayansi na kifikra,

Inaelezwa kuwa hii yote ni katika kuifanya SUZA kuendeleza azma yake ya kuwa kichocheo cha mabadilliko ya jamii.

Gazeti hili limefanya mazungumzo na Makamu Mkuu wa Chuo cha SUZA, Profesa Moh'd Makame Haji kuhusiana na uanzishwaji wa Kigoda hicho na mambo kadhaa mengine. Na haya yalikuwa majibu yake:-

**Kigoda kina jukumu gani la msingi?**

Kigoda hicho kitakasimiwa jukumu la msingi la kuandaa na kuendesha tamasha la kitaaluma kila mwaka la Sheikh Abeid Karume ikiwa ni sehemu ya kusherehekea na kuenzi mchango wake wa kuleta maendeleo kwa jamii ya kitaifa na kimataifa.

Tamasha hili litakusanya wasomi wa ndani na nje ya nchi, wadau kutoka serikalini, taasisi zisizo za kiserikali, wananchi na wadau wengine kuwasilisha mada, kujadili, na kuchangia uzoefu na mawazo kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo kutokana na mada itakayochaguliwa kwa kila mwaka husika. Tamasha litakuwa na majukumu yafuatayo:-

- Kuandaa na kuendesha mihadhara ya Sheikh Abeid Karume.
- Kufanya tafiti na kutoa machapisho mbalimbali yatokanayo na tafiti, mikutano na makongamano mbalimbali yanayoendeshwa na Kigoda hiki;
- Kuandaa na kuendesha mikutano na makongamano ya kitaifa na kimataifa yatakayohusisha wasomi na wadau mbalimbali yenye lengo la kujadili na kueneza falsafa za mchakato endelevu wa ukombozi na maendeleo ya Zanzibar, Tanzania na Afrika kwa ujumla;
- Kuanzisha mashirikiano na vigoda vingine na wadau mbalimbali wa maendeleo ndani na nje ya nchi;
- Kukusanya na kuhifadhi kazi mbalimbali za Sheikh Abeid Amani Karume zikiwemo kumbukumbu za hotuba, mihadhara/mikutano, machapisho, picha cha matukio mbali mbali ya utekelezaji wa harakati za ukombozi na maendeleo katika maktaba maalum itakayoanziswa na Kiti hiki;
- Kuimarisha masomo ya historia na urithi wa kale, akiolojia na stadi za kimaendeleo na kuanzisha masomo yanayoendana na Kigoda hiki katika ngazi zote za elimu;
- Kufundisha kozi za shahada za awali na nyingine na kusimamia tafiti za wanfunzi katika ngazi mbalimbali; na

Kuandaa na kutekeleza mipango na kazi za kila siku za Kigoda ikiwemo programu za kuelimisha, kushajihisha na kuenzi kwa vitendo fikra na falsafa za Sheikh Abeid Amani Karume.



Makamu Mkuu wa Chuo cha SUZA, Profesa Moh'd Makame Haji.

**Kigoda kinawalenga akina nani?**

Walengwa ni wa Kigoda cha Sheikh Karume ni jamii yote ya Kitanzania na ulimwengu wa ujumla na manufaa yatakayopatikana.

**Na ni kwanini iwe sasa na haikuwa wakati mwingine wowote ule.**

Nchi ikiwa imesheherekea miaka sitini ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na tunasheherekea miaka Sitini ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Chuo kimeona ni wakati sasa umefika wa kumuenzi jemedari huyu ambaye ameifanyia makubwa nchi yake na sisi ili kuenzi fikra zake.

**Pengine SUZA ina washirika wengine katika uanzishwaji wa Kigoda hicho.**

Kigoda cha Taaluma cha Hayati Sheikh Abeid Amani Karume kinaanzishwa rasmi na SUZA ingawa Timu ya wanataaluma wa Chuo walipata nafasi ya kwenda kujifunza kwa wenzetu ambao wameanzisha kitu kama hiki kabla yetu. Tunayo mahusano ya mashirikiano na Taasisi nyinginezo.

**Wazo la kuanzishwa kigoda hicho limetokana na nini?**

Wazo la kuanzishwa limetokana na azma ya Chuo kuyaenzi maisha na fikra za Sheikh Abeid Amani Karume ambaye amekuwa ni miongoni mwa wanaharakati na wanamapinduzi wakubwa waliopambana kwa nguvu zote kuhakikisha Zanzibar na Afrika kwa ujumla inakuwa huru ili kuweza kujiletea maendeleo yake kiuchumi.

**Kupitia Kigoda hicho, nini kinaweza kubadilika na tofauti na ilivyo sasa?**

Kama jina la Kigoda lilivyo ni cha Kitaaluma kuna mambo mengi yatabadilika na kuleta tija kwenye taasisi, nchi na jamii kwa ujumla

i. Kutakuwa na tafiti zinafanywa kupitia kigoda. Tafiti ambazo zitakuwa na lengo la kutafuta fumbuzi za changamoto zinazoikabili jamii yetu kisiasa, kiuchumi, elimu na kijamii.

ii. Tunatarajia kigoda kuwa taasisi kubwa inayojitegemea itakayosaidia kutafuta fedha kwa ajili ya kusaidia jamii ikiwemo utoaji wa ufadhili wa masomo kwa wenye uhitaji na kuendeleza harakati za kujikomboa kifikra.

iii. Kupitia Kigoda hiki cha Kitaaluma tunatarajia kuwa na mijadala na makongamano mbalimbali yatakayoibua fursa nyingi kwa vijana ambao ndiyo taifa linalotegemewa kwenye kusaidia maendeleo ya nchi.


## CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

*Kichocheo cha Mabadiliko ya Jamii*

**KUMBUKUMBU YA MIAKA 52 YA KIFO CHA RAIS WA KWANZA WA ZANZIBAR HAYATI SHEIKH ABEID AMAN KARUME 7 APRILI, 1972 – 7APRILI, 2024**

Baraza la Chuo, Menejimenti na Wanajumuiya wote wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar inaungana na wazanzibar na watanzania kwa ujumla katika maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 52 ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Zanzibar na Makamu wa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Sheikh Abeid Aman Karume.

Daima ataendelea kukumbukwa kwa mchango wake mkubwa wa kulikomboa taifa na kulijenga ambapo mpaka sasa bado maono yake ya kuitaka Zanzibar kuwa kitovu cha Maendeleo yanaendelea kuishi.
Aidha Chuo kinaahidi kuyaenzi maono hayo na kutekeleza falsafa zake kivitendo katika kuleta ustawi wa wananchi kijamii na kiuchumi. Katika kulitekeleza hilo, Chuo kinatarajia kuzindua rasmi Kigoda cha Kitaaluma cha Hayati Sheikh Abeid Amani Karume mwaka huu kama kielelezo cha kutunza na kuyafanyia kazi mengi mazuri aliyotuachia.

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinaendeleza juhudi za kutimiza wajibu wake wa kuchangia maendeleo ya elimu nchini na kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii kupitia utoaji wa elimu bora.
Kwa taarifa zaidi kuhusu Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar tembelea tovuti

**http:// www.suza.ac.tz**

**Mawasiliano yote rasmi na Chuo yafanywe kupitia kwa:**

**Makamu Mkuu wa Chuo**
**Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar**
**Sanduku la Posta 146**

**192 Barabara ya Tunguu**
**Zanzibar, Tanzania**
**Barua pepe: vc@suza.ac.tz**

